JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI MALAGARASI,
S.L.P 109,
KIBONDO.

11/05/2018.

Mawasiliano:
Email: malagarasiss@yahoo.com
Mkuu wa shule: +255 752 553 075
M/Mkuu wa shule: +255 755 296 353

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MALAGARASI HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBONDO MKOA WA KIGOMA MWAKA 2018

1.0 Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2018 tahasusi ya…….. shule ya Sekondari malagarasi ipo umbali wa kilometa moja na nusu (1.5 km) mashariki mwa mji wa Kibondo . Usafiri wa bodaboda unapatikana kutoka kituo cha mabasi hadi shuleni na nauli ni shilingi elfu moja (Tshs 1,000) na taksi ni shilingi elfu tatu (Tshs 3,000/=)

Muhula wa kwanza wa msomo kwa wanafunzi wa kidato cha tano utaanza tarehe 03/07/2018, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 02/07/2018 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 16/07/2018.

2.0 **Mambo muhimu ya kuzingatia:**

2.1Sare ya shule

a) Sare za shule hii ni sketi Mbili (2) za rangi ya damu ya mzee kwa wasichana (sketi iwe ndefu hadi ikutane na viatu, kitambaa kizito na sio cha sukari sukari) na suruali mbili za rangi ya damu ya mzee kwa wavulana.

		
Rangi ya kijani ya skirt	Rangi ya damu ya mzee ya skirt na suruali za darasani	Rangi ya blue ya tshirt

b) Rangi ya hijab ni nyeupe inayofunika mikono
c) Sare za michezo kwa shule hii ni truck suit za rangi ya blue/nyeusi na raba za michezo.
d) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
e) Soksi jozi mbili nyeupe za shule.
f) Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali
g) Sweta nyeusi nyenye shingo ya V kwa mbele.
h) Nguo za kushindia (yaani shamba dress) ni sketi mbili za rangi ya kijani cha mgomba kwa wasichana na tshirt ya rangi ya bluu na suruali mbili za rangi

nyeusi kwa wavulana na Tshirt za rangi ya bluu. (sampli za rangi ya vitambaa zimeambatanishwa)

i) Tai ya rangi ya damu ya mzee yenye michirizi myeupe (zinapatikana shuleni kwa gharama nafuu)

2.2Ada na michango ya shule

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000.00 kwa mwanafunzi wa bweni. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35, 000.00 kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule Namba **51501100015,** Jina la akaunti: **Malagarasi Secondary School Contrib Account, NMB Tawi la KIBONDO. (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye bank pay in slip).**

b) Michango Inayotakiwa Kulipwa na Kila Mzazi

i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha
iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
iv. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine
v. Shilingi 2,000/= kwa ajili ya nembo ya shule
vi. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza na bima ya afya. Bima ya afya shilingi 5,000/= na huduma ya kwanza ni shilingi 5,000/=
vii. Shilingi 20,000/= mitihani ya kujipima (mock)
viii. Fedha ya tahadhari shilingi 5000/=(haitarejeshwa)

Jumla ya ada na michango yote kwa mwanafunzi ni shilingi laki moja na sabini na nane (Tshs 178,000/=)
Angalizo: Michango hii yote ilipwe kwenye account ya shule.

c) Mahitaji Muhimu Ambayo Mwanafunzi Anapaswa Kuleta Shuleni:

i. Ream ya karatasi moja (1) kila mwaka
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi aliyochaguliwa kusoma.
iii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa somo la Biology.
iv. Scientific calculator original (asilia) kwa wanafunzi wa tahasusi za sayansi
v. Oxford Advanced Learners' Dictionary kwa wanafunzi wa tahasusi za sanaa.
vi. Kamusi ya Kiswahili ya TUKI kwa wanafunzi wa somo la Kiswahili
vii. Mashuka pair 2 ya rangi ya pink au blue, blanket moja, chandarua na foronya moja (1) ya rangi ya pink au blue.
viii. Godoro kwa wanafunzi wa bweni (godoro liwe na vipimo vya inch $2\frac{1}{2}$x6)
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
x. Ndoo ndogo mbili zenye mifuniko.
xi. Kwanja moja (1) na mfagio mmoja (1) kwa wasichana na jembe moja (1) na mfagio mmoja (1) kwa wavulana. (mfagio wa chelewa)

3.0MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULENI

i. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
ii. Wizi
iii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro

iv. Kugoma na kuhamasisha mgomo
v. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu/walezi na jamii kwa ujumla
vi. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule
vii. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
viii. Kufuga ndevu
ix. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
x. Uvutaji wa sigara
xi. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa
xii. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
xiv. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
xv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4.0VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU

A. FOMU YA HISTORIA YA MWANAFUNZI (Ijazwe na kurudishwa shuleni)
B. FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE (Ijazwe na kurudishwa shuleni)
C. MEDICAL EXAMINATION FORM (ijazwe na kurudishwa shuleni)

KARIBU SANA MALAGARASI SEKONDARI

HEADMASTER
MALAGARASI SEC. SCHOOL
P.O.Box [illegible] SIMBANDO

ADOLF NICODEMUS
MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI MALAGARASI
S.L.P 109 KIBONDO, SIMU: 028 2820171
FOMU NAMBA 1 HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi……
2. Jina la baba ……
3. Jina la Mama……..
4. Jina kamili la mlezi……..
5. Anuani ya mzazi/mlezi……..
6. Uhusiano wa mlezi……..
7. Kazi ya baba (mkulima, mfanyabiashara, mfanyakazi)……
8. Kama ni mkulima zao muhimu analolitegemea ni……
9. Kama ni mfanyabiashara, biashara yake ni……
10. Kama ni mfanya kazi, kazi yake ni……
11. Afya ya mwanafunzi, kama anayo matatizo ya kiafya na hivyo kustahili huduma maalum. Tafadhali mzazi/mlezi aeleze wazi ……
    ……
    ……
12. Madhehebu ya dini……
13. Jamaa na ndugu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya mzazi/mlezi.

Jina Kamili Kazi Yake Namba ya simu a) …… ……. ……

SHULE YA SEKONDARI MALAGARASI
S.L.P 109 KIBONDO, SIMU: 0282820171
FOMU NAMBA 2 FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Jina la mwanafunzi.....
Jina la mzazi/mlezi.....
Anuani ya mzazi/mlezi.....
Uhusiano..... (mjomba, shangazi, kaka, dada).
Mimi .....nikiwa nimechaguliwa kuwa mwanafunzi wa Tanzania naamini kuwa nimetunukiwa nafasi hiyo niliyopewa na umma wa Tanzania. Hivyo naahidi kuwa nitajibidiisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zote nitakazopewa hapa shuleni nje na ndani ya darasa ili kuleta ufanisi. Ili kutimiza shabaha hiyo ninakubali na ninaahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitafanya kazi kwa **BUSARA, JUHUDI YA HALI YA JUU KABISA NA UTII** kwa viongozi wote wa shule pamoja na sheria. Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia na taratibu zinazokubalika.

Sahihi ya mwanafunzi.....tarehe.....

Mimi .....mzazi/mlezi wa mwanafunzi .....ninaahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wa mtoto huyo kwa kushirikiana na shule.

Sahihi ya mzazi/mlezi.....tarehe.....

MALAGARASI SECONDARY SCHOOL
P.O BOX 109 KIBONDO, TEL: 028 2820171
FORM NUMBER 03 MEDICAL EXAMINATION FORM

Pupil's name……
Age ……
Stool test……
Blood group……
Urine analysis……
Sphills test ……
Chest test……
Speech……
Eye test ……
Abdomen……
Additional information and physical defect or impairment to pursue further studies
……
……
……
……
……
……
……
Signed by ……
Designation ……

Official stump
Date ……